# CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO NGOME

**NGOMESACCOS LIMITED**

**DSR 991**

# SERA YA UHAMASISHAJI WA UWEKAJIHISA, AKIBA NA AMANA

**TOLEO LA I: 2020**

**CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO NGOME**

**NGOMESACCOS LIMITED**

**DSR 991**

# SERA YA UHAMASISHAJI WA UWEKAJIHISA, AKIBA NA AMANA

**TOLEO LA I: 2020**

## YALIYOMO

UKURASA


SEHEMU YA KWANZA ........ 3
UTANGULIZI ........ 3- 4
SEHEMU YA PILI ........ 4
HISA ........ 4- 6
SEHEMU YA TATU ........ 7
AKIBA ........ 7- 8
SEHEMU YA NNE ........ 9
AMANA ........ 9-11
SEHEMU YA TANO ........ 11
UHUISHAJI NA UIDHINISHAJI WA SERA ........ 11

## SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.1 Historia

NGOME SACCOS Ltd yenye nambari ya usajiri DSR 991ilisajiriwa tarehe 30 April, 2007 chini ya Sheria ya Ushirika Na 20 ya mwaka 2003 kama ilivyorejewa na Sheria ya sasa ya Ushirika Na 6 ya mwaka 2013 na baadae Sheria mpya ya huduma ndogo za Fedha Na 10 ya mwaka 2018 kama ushirika wa fedha wenye ukomo wa dhima ili kutoa huduma za akiba na mikopo kwa Wanachama wake. Wanachama wa NGOME SACCOS Ltd ni Maafisa, Maaskari, Wastaafu pamoja na Watumishi wa Umma wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la KujengaTaifa na wale walio hamia wizara nyingine wakiwa wanachama Hai wa Ngome SACCOS.

Lengo la kuanzisha NGOME SACCOS Ltd ni kuhamasisha uwekaji akiba na rasilimali fedha na kutoa huduma mbalimbali za kifedha kwa gharama nafuu na kwa wakati mwafaka. Kwa kuzingatia dhana kuwa Wanachama wa NGOME SACCOS Ltd ndiyo wateja wa huduma zinazotolewa, SACCOS inahakikisha menejimenti thabiti ya rasilimali ili kuwapa wanachama faida shinda ni katika uwekezaji wao ndani ya chama. Hii imewezesha Chama kuwa na aina mbalimbali za huduma za akiba, amana na mikopo kwa urahisi wa wanachama kuchagua.

Ofisi za Chama zipo Mwenge Mlalakuwa Barabara ya Bagamoyo, mkabala na Suma JKT.

## 1.2 Madhumuni ya kuwa na Sera hii

Madhumuni ya Sera hii ni kuwa muongozo wa kuwawezesha Wanachama kumiliki Chama chao kwa kununua hisa na kujiwekea akiba katika mazao mbalimbali yatolewayo Chamani.

# SEHEMU YA PILI

# HISA

## 2.1 Maana ya Hisa

Sheria ya Ushirika na. 6 ya mwaka 2013 kupitia kifungu cha 41 inatambua uwepo wa Mwanachama (member) na Mteja (client), ikiwa mwanachama ni yule aliyenunua hisa ndani ya chama wakati mteja ni yule anayetumia huduma za akiba na amana ndani ya Chama.

Hisa ni uwekezaji wa msingi kabisa kwa Mwanachama. Hisa humfanya mwanachama kuwa mmiliki halali wa SACCOS na kumuwezesha kupata Magawio yanayotokana na faida za chama na magawio hayo yatalipwa kulingana na idadi ya Hisa anazomiliki mwanachama.

## 2.2 Aina za Hisa

Kuna aina mbili za hisa ambazo mwanachama anaweza kuchangia ambazo ni;

(i) Hisa za lazima / Msingi.

(ii) Hisa za ziada / hiari.

Hisa za lazima ndiyo hisa za umiliki wa Chama, ni kiwango cha chini cha hisa ambazo kila mwanachama anatakiwa kumiliki ndani ya Chama. Hadi sasa hisa za msingi kwa NGOME SACCOS Ltd ni kumi (10) ambapo kila moja inathamani ya Tsh 10,000/=.

Hisa za ziada ni zile ambazo mwanachama atachangia juu ya hisa za msingi

## 2.3 Ulipaji wa Hisa

Mwanachama wa NGOME SACCOS atatakiwa kulipia hisa zake zote kumi (10) za msingi pale anapojiunga na Chama au kulipia kidogo kidogo ndani ya miezi Sita.

## 2.4 Ukomo wa Hisa kwa Mwanachama

Mwanachama wa NGOME SACCOS hatoruhusiwa kumiliki zaidi ya 1/5 au asilimia 20% ya hisa zote kwenye chama.

## 2.5 Kupunguza Hisa

Hisa za msingi haziwezi kupunguzwa wala kuchukuliwa hadi pale mwanachama atakopokuwa ameacha uanachama ama katika tukio la kifo. Kwa upande mwingine, hisa za hiari zinaweza kuchukuliwa ama kupunguzwa. Endapo kiwango cha hisa za hiari kinachochukuliwa ni kikubwa kuliko kiwango kilichowekwa katika Masharti ya Chama basi Mwanachama atatakiwa kutoa notisi ya siku 14.

## 2.6 Taratibu za kuthibitishwa kuwa Mwanachama

Mwanachama mpya atajaza fomu ya maombi ya uanachama na kulipia hisa zake za msingi kisha maombi yake yatajadiliwa na bodi katika moja ya vikao vyake na maombi hayo yakipitishwa yatapelekwa pia katika Mkutano Mkuu, baada ya maombi kupitishwa kwenye Mkutano Mkuu ndiyo Mwanachama atakua amethibitishwa rasmi kwenye Chama.

## 2.7 Haki ya kupatiwa huduma

Mwanachama atakua na haki ya uanachama na sifa ya kupatiwa huduma za Chama pale tu atakapokuwa amelipia hisa zake zote za msingi na kulipa michango yake ya akiba ya kila mwezi. Haki za uanachama ni pamoja na kualikwa kuhudhulia Mkutano Mkuu na kupatiwa huduma za mikopo.

### 2.9 Uhamishaji wa Hisa

Hisa za msingi haziwezi kuhamishika. Mwanachama anaruhusiwa kuhamisha hisa zake za ziada kwenda kwenye akiba zake kama atataka kujazia akiba kwa ajili ya kuongeza uwiano wake wa akiba na mkopo.

### 2.10 Hisa kuwa Dhamana ya Mkopo

Mwanachama anaweza kutumia hisa za hiari kama dhamana ya mkopo isipokuwa Hisa za msingi haziwezi kutumika kama dhamana ya mkopo kwa mujibu wa Sheria ya vyama vya Ushirika Na 6 ya Mwaka 2013 na kanuni zake.

### 2.11 Cheti cha Hisa

Kila mwanachama anayemaliza kulipia hisa zake zote atapewa cheti cha hisa kuthibitisha umiliki wake kwenye SACCOS. Cheti cha hisa kinaweza kubadilishwa walau baada ya mwaka mmoja kutokana na ongezeko la thamani za hisa alizonazo Mwanachama au mabadiliko yoyote yanayoweza kujitokeza ndani ya Chama.

### 2.12 Hisa Kushikiliwa kama Mali katika mchakato wa Ufilisi

Kifungu cha 63 cha Sheria ya Ushirika na. 6 ya mwaka 2013 inakataza hisa za mwanachama kushikiliwa (attachment) kama mali za mdaiwa wakati wa mchakato wa ufilisi

### 2.13 Kuacha Uanachama

Endapo mwanachama ataacha uanachama kwa sababu yoyote ile Chama hakitarudisha hisa za msingi kupitia kasma ya hisa za Chama isipokuwa Chama kitamrejeshea hisa zake kupitia fedha zilizoko katika tengo la kukombolea mafungu.

Endapo Chama hakina fedha za kutosha kwenye kasma ya tengo la kukombolea mafungu, mwanachama ataruhusiwa kuuza hisa hizo kwa mwanachama mwingine au kama Chama kitakua katika hali nzuri ya ukwasi basi kitanunua hisa hizo ili kumpatia fedha mwanachama aliyeacha uanachama na kuziuza kwa mwanachama mwingne mpya au anayeendelea.

### 2.14 Mwanachama Sinzia

Chama kitachukulia mwanachama sinzia endapo hakuna muamala wowote umefanyika ndani ya kipindi cha mwaka mmoja. Pia chama kitachukulia akaunti kuwa imeachwa baada ya miaka 5 bila kupokea mawasiliano yoyote kimaandishi kutoka kwa mwanachama mwenyewe au mrithi wake, fedha katika kasma hii zitatolewa na kuwekwa kwenye kasma maalum ya tengo la Hisa zilizoachwa.

Endapo mwanachama au mrithi wake atajitokeza basi fedha hizo zitarejeshwa baada ya kujiridhisha uhalali wa mrithi na kwa mujibu wa taratibu na sheria.

## SEHEMU YA TATU

## AKIBA

### 3.1 Utangulizi

Akiba ni fedha anazochangia mwanachama ili kuwa na sifa ya kupata huduma za mikopo.

### 3.2 Aina ya Akiba

NGOMESACCOS Ltd itakuwa na makundi makuu mawili(2) ya Akiba

(i) Akiba ya lazima.

(ii) Akiba ya hiyari.

Akiba ya lazima inamfanya mwanachama kuwa na sifa ya kupata huduma ya mikopo na akiba hii haita cheza cheza kwa maana ya kutoka ama kupungua kama inavyo elekezwa kwenye Masharti ya Chama. Akiba hii itakuwa ni kiasi kisichopungua Tsh 50,000/= kwa mwezi.

Akiba ya hiyari ni akiba anayojiwekea mwanachama kwa malengo mahususi na akiba hii inaweza kutolewa ama kupunguzwa muda wowote.

Kwa mwanachama anayetaka kujiunga na kupata huduma ya mkopo wa Dharula atahitajika kulipa fedha taslim kwa ajili ya michango ya akiba ya miezi mitatu.

Mwanachama asiyechangia akiba kwa kipindi cha miezi mitatu mfululizo atahesabika kuwa ni Mwanachama asiye hai.

### 3.3 Aina ya Mazao ya Akiba ya Hiyari

Mwanachama anaweza kuweka akiba yake ya hiyari katika moja ya mazao yafuatayo:-

i. Akiba ya Malengo Maalum
ii. Akiba ya Wastaafu
iii. Akiba ya Mshahara

Chama kitaendelea kubuni mazao mengine ya Akiba ili kuwahamasisha wanachama waweze kuweka Akiba zaidi

### 3.4 Riba Juu ya Akiba

Kila mwaka NGOMESACCOS Ltd kupitia Mkutano Mkuu itaweka kiwango cha riba juu ya akiba za wanachama ili kuwezesha ongezeko la thamani ya akiba hizo. Kwa kuwa hii ni gharama ya kifedha kwenye Chama, itakuwa inabadilika kila mwaka kutokana na mwelekeo wa makisio ya mapato na matumizi pamoja na faida inayopatikana. Hata hivo, faida juu ya akiba itakuwa ndani ya uwiano wa asilimia 3-17(3%-17%).

Kiasi hi kikitaingizwa moja kwa moja katika akaunti ya akiba ya mwanachama baada ya kukatwa kodi ya zuio (Withholding Tax).

### 3.5 Kupunguza Akiba

Mwanachama anaweza kupunguza akiba yake kwa vigezo vifuatavyo;-

i. Akiba iwe huru.
ii. Awe amechangia akiba kwa muda usiopungua miezi 36.
iii. Apunguze ½ au asilimia 50% ya akiba huru.
iv. Anaweza kupunguza akiba mara moja kila baada ya miaka 3.
v. Mwanachama ambaye akiba zake zimetokana na Mkopo hataruhusiwa kupunguza Akiba mpaka mkopo husika utakapomalizika.

### 3.6 Kukoma Uanachama

Mwanachama akikoma kuwa mwanachama wa NGOME SACCOS Ltd atatakiwa kuandika notisi na akiba zake atarejeshewa ndani ya siku 90 tokea kupokelewa kwa notisi hiyo na kutegemeana na hali ya Ukwasi wa chama.

## SEHEMU YA NNE

## AMANA

### 4.1 Utangulizi

Amana ni fedha anayoiweka mwanachama kwa lengo la kujiwekea akiba inayoweza kumsaidia badae. Amana ni fedha inaweza kuwekwa muda wowote na kutolewa amakupunguzwa muda wowote.

### 4.2 Aina za Amana

Ili kuendesha Chama kibiashara, NGOME SACCOS Ltd inaweza kuongeza zao lingine la amana ili kuwawezesha Wanachama kuweka na kuchukua fedha kwa urahisi katika Chama chao, endapo Bodi itaona inafaa kuwa na zao hilo. Yafuatayo ni makundi 2 makuu ya aina za amana ambazo ni;-

(i) Amana za Kawaida
(ii) Amana za Muda Maalum

Amana za kawaida ni fedha anayoiweka mwanachama muda wowote na anaweza kuitoa muda wowote anapohitaji.

Kwa upande mwingine amana za muda maalum ni amana ambazo Mwanachama anaingia makubaliano au mkataba na Chama kutoichukua amana yake kwa muda uliokubaliwa kwa ahadi ya Chama kumlipa riba ndani ya kipindi cha makubaliano. Viwango vya riba katika amana za muda maalum vitatokana na hali ya biashara pamoja na viwango vya soko la fedha.

## 4.3 Taratibu za Uwekaji Amana

Chama kitakuwa na fomu maalum kwa ajili ya Mwanachama kujaza na kuweka amana. Kutakuwa na fomu tofauti za Amana za kawaida na amana za muda maalum.

Kutokana na maendeleo ya TEHAMA mwanachama anaweza kupokea/kutoa fedha zake za amana za kawaida kwa kutumia simu yake ya kiganjani. Amana hiyo ikipokelewa itaingizwa kwenye reja kadi ya mwanachama husika na stakabadhi kuandikwa.

## 4.5 Cheti cha Amana za Muda Maalum

Mwanachama aliyeweka amana ya muda maalum atapewa cheti **(certificate of deposit);**cheti hicho kitakuwa na tarehe ya kuweka na kuiva, jina la mwanachama, kiwango cha fedha zilizoweka, riba,kodi ya zuio, muda na saini ya Meneja.

## 4.6 Kuvunja Mkataba

Endapo mwanachama atavunja mkataba yaani anahitaji fedha zilizo kwenye amana ya muda maalum kabla ya muda wa kuiva kufika atarejeshewa pesa yake bila riba.

## SEHEMU YA TANO

### HITIMISHO

Sera hii imeandaliwa na Bodi ya Ngome SACCOS na Kamati ya Usimamizi iliyokasimiwa madaraka kwa niaba ya wanachama kwa barua yenye kumbukumbu Na. MA.82/309/20/14 ya tarehe 05 AGOSTI, 2020 na itaanza kutumika baada ya kuidhinishwa na Mrajis

Mwenyekiti

Katibu

TANZANIA
Approved this 01ST
day of MARCH 2021
Asst. Registrar of Cooperative Societies